USAFIRI ARDHINI

ISSN 2961 - 6255

JULAI - SEPTEMBA, 2025

Toleo la 08

LATRA YANG'ARA TUZO YA UTOAJI HUDUMA BORA

Uk.. 1

LATRA YANG'ARA TUZO YA UTOAJI HUDUMA BORA

Tuzo hiyo imetolewa Agosti 24, 2025 na Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kupokelewa na Prof. Ahmed Ame, Mwenyekati wa Bodi ya LATRA akiambatana na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu.....

LATRA KUADHIMISHA WIKI YA USAFIRI ENDELEVU ARDHINI

"Maadhimsho hayo yatakuwa na midahalo ya kisera, makongamano, mijadala ya kitaalamu na maonesho yatayojumuisha sekta binafsi, taasisi za kiserikali jumuiya za kikanda na kimataifa pamoja na wadau wa usafirishaji barabara, reli na waya kwa lengo la....."

Uk... 2

LATRA, DCEA KUSHIRIKIANA KUDHIBITI USAFIRISHAJI WA DAWA ZA KULEVYA

"Tunatoa elimu kwa madereva, makondakta na wamiliki wa magari ili waelewe kwamba wanapokamatwa na dawa za kulevya kupitia basi au chombo cha moto anachoendesha, dereva na kondakta wanahusika.....

Uk... 17

SAFARI Tiketi TANZANIA

LATRA
IMETHIBITISHWA ISO 9001

CPA HABIBU SULUO
MKURUGENZI MKUU - LATRA

Maendeleo ya sekta ya usafiri ardhini yanategemea sana jitihada za kila mmoja wetu bila kusahau Serikali ambayo ndiye msimamizi mkuu anayehakikisha huduma na uendeshaji wa sekta unakuwa zenye tija na manufaa kwa wote. Kwa kuzingatia hili, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inafanya kila linalowezekana kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji nchini.

Hili ni toleo la nane la jarida la USAFIRI ARDHINI ambalo limeakisi jitihada zinazotekelezwa ili kurahishisha utoaji na upatikanaji wa huduma za usafiri ardhini nchini na limekusanya taarifa zilizoandaliwa na kuhaririwa kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2025.

Ndani ya jarida hili utafahamu mafanikio ya LATRA katika sekta ndogo tatu zinazodhibitiwa yaani sekta ndogo ya usafiri wa barabara, usafiri wa reli na usafiri wa waya ambapo mafanikio haya ni yametokana na jitihada za kutekeleza majukumu kwa uweledi, ufanisi huku tukitimiza maono ya Serikali ya kuwa na usafiri ardhini ulio bora na salama.

Miongoni mwa taarifa zinazopatikana kwenye jarida hili ni pamoja na Agosti 24, 2025 Mamlaka ilikabidhiwa tuzo na Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuibuka mshindi wa pili miongoni mwa taasisi za Serikali zinazotoa huduma bora na zisizofanya biashara ikiwa ni sehemu ya Serikali kutambua mchango mkubwa wa LATRA katika kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini na kuhakikisha wananchi wanapata huduma salama, bora na zenye uwazi.

Vilevile Wizara ya Uchukuzi imetangaza rasmi kuwa, kwa mara ya kwanza Tanzania inaenda kuadhimisha Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini itakayofanyika Novemba 24 hadi 29, 2025 Jijini Dar es Salaam itakayowakutanisha wadau zaidi ya 1,000 kutoka ndani na nje ya nchi watakaojadili kwa pamoja namna bora ya kuboresha sekta ya usafiri ardhini nchini pamoja na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wadau.

Pia LATRA imeendelea kuhakikisha huduma zinatolewa kwenye mabasi ya masafa marefu zinazingatia Sheria za nchi. Katika kufanikisha hilo, LATRA inashirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) katika utoaji wa elimu ya namna bora ya kudhibiti vitendo vya usafirishaji wa dawa za kulevya kwa wamiliki wa mabasi ya masafa marefu, madereva na wahudumu ambapo wamekuwa wakisafirisha bidhaa hizo kwa kujua au bila kujua.

Nikukaribishe sasa usome yaliyojiri katika jarida hili, naamini utahabarika na kujifunza. Mamlaka itaendelea kusimamia sekta inazozidhibiti kwa mujibu wa Sheria na kuhakikisha wadau wote wa usafiri ardhini wananufaika na sekta yao. Kwa maoni yoyote, usisite kuwasiliana nasi kwa namba zetu bila malipo 0800110019 / 0800110020 au kupitia Mfumo wa e -mrejesho unaopatikana kwa anwani https://emrejesho.gov.go.tz/ au kwa kufika ofisi ya LATRA iliyo karibu yako. Pia, tutumie ushahidi wa video na picha zinazohusu uvunjifu wa Sheria za Usafiri Ardhini kwa namba ya WhatsApp 0681300800, nasi tutazifanyia kazi kwa wakati.

Nikutakie usomaji mwema wa jarida hili
"Pamoja kwa Usafiri Bora"

LATRA YANG'ARA TUZO YA UTOAJI HUDUMA BORA

Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wa tatu kulia) akikabidhi tuzo yamshindi wa pili miongoni mwa taasisi za Serikali zinazotoa huduma bora na zisizofanya biashara kwa Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi LATRA (wa pili kulia) Agosti 25, 2025 Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) katika kikao kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeibuka mshindi wa pili miongoni mwa taasisi za Serikali zinazotoa huduma bora na zisizofanya biashara ikiwa ni sehemu ya Serikali kutambua mchango mkubwa wa LATRA katika kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini.

Tuzo hiyo imetolewa Agosti 24, 2025 na Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kupokelewa na Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya LATRA akiambatana na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA katika kikao kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma kilichoratibiwa na ofisi ya Msajili wa Hazina na kufanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC)

Aidha tuzo hiyo imetolewa kwa kuzingatia vigezo vya utawala bora, uboreshaji wa huduma, matumizi ya mifumo ya kidigiti kiwango cha kuridhika kwa wateja pamoja na ongezeko la wananchi wanaonufaika na huduma za LATRA.

LATRA inaendelea kuboresha mifumo, kuongeza ubunifu na kushirikisha wadau ili kuhakikisha wananchi wanafurahia huduma bora, salama na zenye viwango. ushindi huu umechagizwa na jitihada zinazotekelezwa na Bodi ya Wakurugenzi LATRA, Menejimenti pamoja na watumishi wa Mamlaka.

LATRA
IMETHIBITISHWA ISO 9001

LATRA KUADHIMISHA WIKI YA USAFIRI ENDELEVU ARDHINI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi inatarajia kuadhimisha maadhimisho ya kwanza ya wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini 2025 kuanzia Mwezi Novemba 25 hadi 29, 2025 Mkoani Dar es Salaam.

Amebainisha hayo Bw. Benjamin Mbimbi, Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Usafiri wa Reli Wizara ya Uchukuzi aliyemuwakilisha Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Uchukuzi katika kikao cha pili cha maandalizi ya Wiki ya Usafiri Ardhini Endelevu 2025 kilichoandaliwa na LATRA nakufanyika Agosti 29, 2025 ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA Dar es Salaam.

"Wizara ya uchukuzi kwa kushirikiana na LATRA imeanza maandalizi ya maadhimisho ya kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini kimataifa ambapo kupitia azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN) lililopitishwa Mei 16, 2023 kupitia uamuzi namba 77/286, ulioanzisha siku ya usafiri ardhini endelevu duniani (World Sustainable Transport Day) ambayo huadhimishwa 26 kila mwaka na kwa mamlaka tuliyonayo kwa kushirikiana na wadau wa usafirishaji tunaadhimisha kwa mara ya kwanza maadhimisho haya kwa kauli mbiu isemayo Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji" amesema Bw. Mbimbi.

Kwa upande wake CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa maadhimisho hayo yataleta pamoja wadau wa sekta ya usafiri wa ardhini kutoka ndani na nje ya nchi ili kujadili namna ya kuboresha mifumo ya usafiri salama, shirikishi na rafiki kwa mazingira.

"Maadhimsho hayo yatakuwa na midahalo ya kisera, makongamano, mijadala ya kitaalamu na maonesho yatayojumuisha sekta binafsi, taasisi

Inaendelea >>> Uk 3

LATRA KUADHIMISHA WIKI YA USAFIRI ENDELEVU ARDHINI

<<< Inatoka Uk 2

za kiserikali jumuiya za kikanda na kimataifa pamoja na wadau wa usafirishaji barabara, reli na waya kwa lengo la kuwaleta pamoja wadau wote wa sekta ya usafiri ardhini na kuunda malengo ya pamoja ya utekelezaji ili huduma ya usafirishaji iboreshwe iwe salama na rafiki kwa mazingira na yenye tija kwa kizazi cha sasa na Kijacho" amesema CPA Suluo.

CPA Suluo amesema maadhimisho hayo yanaadhimishwa sambamba na juhudi za Serikali za kukuza matumizi ya nishati safi katika usafiri ikiwemo miradi ya mabasi ya mwendokasi yanayotumia gesi asilia (CNG), pamoja na magari ya umeme yanayoanza kuingia sokoni

Kwa upande wake Bw. Chuki Shabani, Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Malori Makubwa na Madogo Tanzania (TAMSTOA) amesema sekta ya usafirishaji imefarijika kupata siku maalum ya kutambua mchango wake.

"Sekta hii ni kubwa kwa muda mrefu tumekuwa hatuna siku yetu sasa tunafarijika kuwa na siku yetu itakayotupa fursa mbalimbali za kushiriki na kujifunza zaidi kuhusu teknolojia katika usafirishaji. niipongeze pia Serikali kwa juhudi za kuleta gesi kama mbadala wa mafuta ili kulinda mazingira na kuongeza mapato ya taifa" amesema Bw. Shabani.

Aidha Bw. Priscus Joseph, Katibu Mkuu Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), ameeleza kuwa dunia inaelekea kupunguza matumizi ya mafuta hivyo nawao hawatakiwi kubaki nyuma.

"tayari tumeshuhudia mabasi ya umeme yakifanya safari kwa gharama nafuu ukilinganisha na yale yanayotumia mafuta kwa mfano basi la umeme linaweza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kwa gharama ya umeme ya takriban Shilingi 15,000/= wakato basi la dizel hutumia zaid ya shilingi 300,000/= kwa safri moja hii itasaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni na kutunza mazingira" amesema Joseph.

Maadhimisho haya yatafanyika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam kwa ajili ya maonesho kuanzia 25 hadi 29 Novemba, 2025 na kwa makongamano yatafanyika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam kuanzia 25 hadi 27 Novemba, 2025 na yatatoa fursa kwa wadau kujifunza teknolojia mpya na namna bora ya kupunguza gharama za uendeshaji.

SAFARI TIKETI YAPAISHA LATRA NANENANE 2025

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetengeneza Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) unaojulikana kwa jina la Safari Tiketi ulioounganishwa na mifumo mingine ya utoaji tiketi ukiwemo wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) na mifumo ya tiketi za mabasi kurahisisha ukataji tiketi na kutunza taarifa sahihi za abiria.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye Maonesho ya 32 ya Kimataifa ya Kilimo Nanenane Agosti 8, 2025 yaliyofanyika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa, jambo lililowavutia watu wengi kwenye maonesho hayo ni matumizi ya Tiketi Mtandao ambapo hadi sasa jumla ya kampuni tano (5) zimekidhi vigezo na kupatiwa vibali vya kutoa huduma za tiketi mtandao baada ya kuthibitishwa na LATRA kuwa mifumo yao ni salama na imezingatia vigezo na masharti.

"Eneo hili tumeendelea kutoa msisitizo na siku za karibuni tumekuwa tukizungumzia kutoa kibali kwa makampuni au mifumo ambayo inatoa tiketi mtandao na ikumbukwe kuwa Serikali ilitoa Kanuni ya kusimamia usafiri huu ambayo ni Kanuni ya 5 ya Kanuni za Tiketi Mtandao za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024 ambazo zimeweka vigezo vya kupata kibali ikiwa ni pamoja na mfumo husika kuwa na ulinzi dhidi ya uvamizi wa kimtandao na kuwa na uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya Serikali" amesema CPA Suluo.

Kwa upande wake Bw. Frank Fredy, Meneja wa Kanda ya Kati wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) amesema kuwa, Mfumo wa Safari Tiketi umeondoa migogoro mingi ya Bima kwa kuwa na uwezo wa kutunza taarifa za abiria kwa mtumiaji wa mfumo huo ambaye anapaswa kujaza taarifa zake kwa usahihi ikiwemo majina kamili, namba ya simu na mahali anapokwenda.

"Mfumo huu wa Safari Tiketi umesaidia sana kutatua migogoro kati ya kampuni za bima na watumiaji wa bima, ilikuwa mtu akikosa tiketi anakosa haki ya kulipwa fidia lakini kwa sasa kwa kutumia mfumo wa safari tiketi unapata taarifa za abiria na analipwa haki yake, hili ni jambo zuri ambalo linampa mwananchi ambae angeweza

Inaendelea >>> Uk 5

SAFARI TIKETI YAPAISHA LATRA NANENANE 2025

<<< Inatoka Uk 4

kupoteza haki yake kupata haki zake za msingi, ninacho sisitiza kwa wananchi ni kwamba hakikisha unapata tiketi yako ya kielektoniki ili tatizo linapotokea safarini uweze kulipwa fidia za bima kwa urahisi" amefafanua Bw. Fredy.

Wakati huohuo Bw. Jabeer John, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Wasafirishaji Mkoa wa Mwanza (UWAMWA), ameeleza kuwa chama hicho kimezindua mfumo wa Tiketi Mtandao kwenye maonesho hayo ya Nanenane ambapo abiria wa mabasi ya mijini (daladala) Mwanza anaweza kukata tiketi hiyo kwa wakala alioko karibu yake na kuitumia anapoingia na kutoka kwenye usafiri huo na kwamba utasaidia kupunguza changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zikiwakabili watumiaji wa usafiri huo na kusaidia serikali kupata takwimu sahihi za watumiaji wa usafiri wa mijini.

LATRA itaendelea kutekeleza kwa ufasaha maagizo ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kubuni na kutumia mifumo ya TEHAMA katika kuimarisha huduma za usafiri ardhini nchini.

KAMPUNI 6 ZA TIKETI MTANDAO ZAPEWA SIKU 14 KUTATUA CHANGAMOTO ZA MIFUMO YAO

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa siku 14 kuanzia Julai 2, 2025 kwa Kampuni sita (06) za Tiketi Mtandao ambazo bado mifumo yao ina changamoto na imezitaka kuzitatua ili kuidhinishwa na watakaoshindwa hawataruhusiwa kuendelea kutoa huduma hiyo.

Amebainisha hayo Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA alipoongea na vyombo vya habari ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA Dar es Salaam Julai 2, 2025.

Bw. Pazzy amezitaja kampuni hizo kuwa ni AB Courier Express Limited, Busbora Company Limited, Logix Company Limited, Mkombozi Infotech Company, Sepatech Company Limited na Web Corporation Limited.

Vilevile Bw. Pazzy ameeleza kuwa, kampuni tatu (03) zimekidhi vigezo na zinaendelea kukamilisha taratibu zingine ili waweze kupatiwa kibali cha utoaji huduma za Tiketi Mtandao.

"Hadi tarehe 30 Juni, 2025, kampuni ya Otapp Agency Company Limited, Hashtech Tanzania Limited na Iyishe Company Limited zimekidhi vigezo vya kupata kibali cha kutoa huduma za Tiketi Mtandao kwa mujibu wa Sheria na Mamlaka imeruhusu kampuni hizo kufanya malipo ili kukabidhiwa vibali vyao," amefafanua Bw. Pazzy.

Aidha ameeleza kuwa, kampuni ya Duarani Innovative Company na

Inaendelea >>> Uk 6

KAMPUNI 6 ZA TIKETI MTANDAO ZAPEWA SIKU 14 KUTATUA CHANGAMOTO ZA MIFUMO YAO

<<< Inatoka Uk 5

Itule Company zimebainika kuwa na changamoto na kukosa sifa za kutoa huduma ya Tiketi Mtandao na hivyo wamepewa siku (07) za matazamio na wakishindwa hawataruhusiwa kutoa huduma na wateja wao watashauriwa kuhamia kwa watoa huduma waliokamilisha utaratibu.

Vilevile amesema, watoa huduma wote wanapaswa kukamilisha na kuendelea kutekeleza matakwa ya kisheria ya kuunganisha mifumo yao na mfumo mkuu wa Tiketi Mtandao (CeTS) ikiwa ni pamoja na kuingiza taarifa za mabasi yote wanayoyahudumia kwenye Mfumo Jumuishi wa Tiketi Mtandao wa Mamlaka (UTS) na watoa huduma wote ambao hawapo katika orodha iliyotajwa hawatambuliki na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria.

Kanuni ya 5 ya Kanuni za Tiketi Mtandao za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024 zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 20 la Januari 12, 2024 zimeweka vigezo vya kupata kibali ambavyo ni pamoja na mfumo husika kuwa na ulinzi dhidi ya uvamizi wa kimtandao na kuwa na uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya Serikali.

Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) (wa katikati) akizungumza na vyombo vya habari ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA Dar es Salaam Julai 2, 2025. Pichani ni Bi. Halima Lutavi, Meneja Ufuatiliaji LATRA (wa kulia) na Bw. Leo Ngowi, Meneja Leseni na Usajili LATRA (wa kushoto)

LATRA
IMETHIBITISHWA ISO 9001

MHE: MBARAWA: ONGEZENI UDHIBITI USAFIRI WA SGR

Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi akisikiliza maelezo kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wakati alipotembelea banda la LATRA kwenye Kongamano la Tatu la Kimataifa la Uchukuzi na Lojistiki lililoandaliwa na Chuo cha Usafirishaji (NIT) Ukumbi wa Mlimani City Dar es Salaam Agosti 21, 2025.

Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuongeza udhibiti wa usafiri wa Reli ya Treni ya Kisasa (SGR) ili kuhakikisha watumiaji wa usafiri huo wanapata huduma bora na salama.

Amesema hayo alipotembelea banda la LATRA kwenye kongamano la Tatu la Kimataifa la Uchukuzi na Usafirishaji Agosti 21, 2025 ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

"Nawaagiza kuongeza udhibiti katika usafiri wa SGR ili kuendelea kuboresha sekta ya usafiri wa reli nchini kwakuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye usafiri huu ambao ni kichocheo cha ongezeko la uchumi wa wananchi na Serikali kwa jumla" amesema Prof. Mbarawa.

Aidha Prof. Mbarawa ameipongeza LATRA kwa utendaji kazi na ubunifu wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambazo zimerahisisha huduma za usafiri ardhini ikiwemo Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) unaojulikana kwa jina la Safari Tiketi unaomuwezesha mwananchi kukata tiketi za usafiri wa mabasi na usafiri wa Treni ya Reli ya kisasa (SGR) na kutunza taarifa sahihi za abiria, Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaopatikana kwa anwani ya ***pis.latra.go.tz*** unaomuwezesha mwananchi kupata taarifa za mabasi yanayowasili katika vituo vya mabasi Tanzania bara na kujua mwenendo wa basi alilopanda.

LATRA imeshiriki Kongamano hilo la siku mbili lililoandaliwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuanzia Agosti 21 hadi 22, 2025 lenye kaulimbiu "Tumia Mifumo Bunifu na Endelevu kwa ajili ya Kuimarisha Usalama wa Sekta ya Usafirishaji"

MAUPIDA YATUNUKIWA CHETI CHA UWAKALA WA LATRA

Mhe. Edward Mpogolo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala ametunuku Cheti cha Uwakala wa kutoa leseni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri ardhini (LATRA) kwa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Maafisa Usafirishaji wa Pikipiki Dar es Salaam (MAUPIDA SACCOS) Agosti 13, 2025 kwenye hafla iliyofanyika ukumbi wa Golden Jubilee, Dar es Salaam.

Akikabidhi cheti hicho kwa niaba ya Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, Mhe. Mpogolo amewapongeza MAUPIDA SACCOS LTD kwa kuwa mawakala rasmi wa LATRA huku akiwasihi kuhamasishana kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo ikiwemo kuhakikisha kila chombo kinachotoa huduma ya usafirishaji kinakuwa na leseni.

"Muhimizane ninyi kwa ninyi kufuata alama za barabarani, kuendesha kwa mwendo unaokubalika kwa mujibu wa Sheria, epukeni kufanya vitendo vinavyohatarisha maisha yenu mkiwa katika kazi zenu na kikubwa zaidi mkumbuke kuwa ninyi ni nguvukazi ya Taifa lakini pia mnategemewa na familia zenu, hivyo usalama unatakiwa kuwa kipaumbele chenu," amesema Mhe. Mpogolo.

Inaendelea >>> Uk 9

Mhe. Edward Mpogolo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala (wa pili kulia) akikabidhi Cheti cha Uwakala wa Kutoa Leseni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Maafisa Usafirishaji wa Pikipiki Dar es Salaam (MAUPIDA SACCOS) Agosti 13, 2025 kwenye hafla iliyofanyika ukumbi wa Golden Jubilee, Dar es Salaam.

MAUPIDA YATUNUKIWA CHETI CHA UWAKALA WA....

<<< Inatoka Uk 8

Vilevile Mhe. Mpogolo amesema cheti cha uwakala wa LATRA walichopatiwa ni alama ya uaminifu, uadilifu na fursa, hivyo wanapaswa kukitumia vizuri ili kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha miradi ya maendeleo itakayowawezesha kutimiza malengo yao kupitia uwakala waliopata kwa kutoa huduma bora na salama za usafiri kwa wananchi.

Aidha Mhe. Mpogolo amebainisha kuwa, yeye kama mlezi atashirikiana nao bega kwa bega ili kuhakikisha ushirika huo unakuwa kinara na wa mfano nchini, "Tutaendelea kushirikiana kwa ukaribu pamoja na wadau wengine ili kuhakikisha mnafikia malengo mliyojiwekea na pia tutahakikisha shughuli za usafirishaji zinafanyika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, na Miongozo iliyopo. Tunataka kuona Pikipiki za magurudumu mawili, matatu, daladala, na watoa huduma wengine wa usafiri ardhini wakifanya kazi katika mazingira yenye mpangilio mzuri, salama na tija kwa jamii na Taifa kwa jumla."

Naye DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara LATRA aliyemuwakilisha CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa, Mamlaka inafanya jitihada ya kuwaunganisha pamoja maafisa usafirishaji kwa kuwapatia elimu na kuwashawishi kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika ambavyo vitawasaidia kuweka akiba na kuwaongezea kipato.

Inaendelea >>> Uk 10

MAUPIDA YATUNUKIWA CHETI CHA UWAKALA WA....

<<< Inatoka Uk 9

"LATRA inalenga kuondoka kwenye utaratibu wa kudhibiti mtu mmoja mmoja na kwenda kwenye mfumo wa udhibiti kupitia vyama vya ushirika au kampuni ambapo wasafirishaji watainuana kiuchumi, kusimamiana wenyewe na kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao wakizingatia masharti ya leseni za usafirishaji walizonazo bila kushurutishwa," ameeleza DCP Kahatano.

Kwa upande wake Bw. Atanas Kitime, Mwenyekiti wa Bodi ya MAUPIDA SACCOS LTD amemshukuru Mhe. Mpogolo kwa kuwa nao bega kwa bega na kuwawezesha kufanikisha uazishwaji wa chama hicho ambao unaenda kubadili maisha yao na pia ameishukuru LATRA kwa kuweka asilimia 20 ya gawio watakalolipata kutokana na leseni watakazozikata.

"Tuna matumaini makubwa kuwa hali zetu za maisha zinaenda kuboreka kupitia ushirika wetu ukizingatia tunaenda kunufaika na 20% ya mapato tutakayokusanya huku tukichangia pato la Taifa. Pia, tutahakikisha ukataji wa leseni za usafirishaji unaongezeka na tutatekeleza majukumu yetu kwa mujibu wa Sheria," amesema Bw. Kitime.

Bw. Said Kagoma, Mwenyekiti wa Shirikisho la MAUPIDA amewataka

"Tutahakikisha shughuli za usafirishaji zinafanyika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, na Miongozo iliyopo. Tunataka kuona Pikipiki za magurudumu mawili, matatu, daladala, na watoa huduma wengine wa usafiri ardhini wakifanya kazi katika mazingira yenye mpangilio mzuri, salama na tija kwa jamii na Taifa kwa jumla."

Mhe. Edward Mpogolo

waendesha bodaboda kuzingatia Sheria za usalama barabarani ikiwemo kuvaa kofia ngumu (helmet) kubeba abiria kwa usahihi na kuendesha kwa uangalifu ili kuepusha ajali ambazo zinaepukika.

MAUPIDA SACCOS LTD wamepatiwa cheti cha uwakala ambacho kitawaruhusu kutoa aina sita za leseni za vyombo vya moto vya kukodi ambazo ni leseni za Pikipiki za Magurudumu Mawili, Leseni za Pikipiki za Magurudumu Matatu, Leseni za Taksi za kawaida, Leseni za Taksi Mtandao (Ride Hailing), Leseni za Magari Maalumu ya Kukodi (Special Hire) pamoja na Leseni za Kuitisha Mtandaoni Usafiri wa Kuchangia (Ride Sharing).

LATRA
IMETHIBITISHWA ISO 9001

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikata utepe kuashiria ufunguzi wa bandari kavu Julai 31, 2025 kwenye hafla ya Ufunguzi wa Bandari Kavu ya Kwala.

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Menejimenti ya LATRA kwenye picha ya pamoja na wafanyakazi wa kampuni ya Superdoll wakati wa ziara ya Bodi ya Wakurugenzi LATRA kwa Kampuni ya Superdoll, Dar es Salaam Agosti 01, 2025.

Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akitoa maelezo kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na LATRA kwa wadau waliotembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nanenane Agosti 8, 2025 Dodoma.

LATRA

JINSI YA KUTUMIA MFUMO WA
LESENI ZA LATRA (RRIMS)

Jisajili kwa kutumia simu yako au kompyuta, kupitia kiunganishi ***rrims.latra.go.tz*** kisha bofya neno ***Get started*** Utaona mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kuendelea.

MTU BINAFSI:

- Bofya ***Jisajili kama mtu binafsi*** kwa kutumia namba ya **NIDA**
- Thibitisha namba hiyo kwa kujibu maswali yatakayoulizwa kwenye mfumo
- Hakiki taarifa zako na jaza maeneo yaliyo wazi.

LATRA

JINSI YA KUTUMIA MFUMO WA
LESENI ZA LATRA (RRIMS)

- Kwa Mabasi ya Abiria (Daladala na Masafa marefu) Chagua ***Vyombo vya Abiria (Public Service Vehicles)***
- Kwa Magari ya mizigo Chagua ***Vyombo vya mizigo (Goods Carrying Vehicles)***
- Kwa Pikipiki, Teksi, Magari Maalum ya Kukodi (Special hire na Rental Cars), Taxi Mtandao, Magari ya Shule (School Bus), na Staff Bus chagua ***Vyombo vya Kukodi (Private Hire Vehicles)***

Ukimaliza kujaza taarifa zote kwa usahihi, thibitisha na **Hifadhi Ombi Lako**

LATRA

JINSI YA KUTUMIA MFUMO WA
LESENI ZA LATRA (RRIMS)

TAASISI:

- Bofya ***sajili Kampuni/Taasisi:*** utatumia namba ya cheti cha Usajili (BRELA/HALMASHAURI)

-Baada ya kujisajili, utatumiwa kiunganishi kwenye baruapepe(e-mail) yako uliyoiweka wakati wa kujisajili.
-Bofya neno ***"Password reset"*** kwa ajili ya kutengeneza **NYWILA** (Password).

Kufanya Maombi:

Ingia kwenye mfumo kupitia akaunti yako (***rrims.latra.go.tz***) kwa kutumia baruapepe (e-mail) na nywila (password) uliyotengeneza.

LATRA

JINSI YA KUTUMIA MFUMO WA
LESENI ZA LATRA (RRIMS)

Baada ya kufanya malipo unaweza kuchapa leseni yako mwenyewe kupitia mfumo.

Kwa Usaidizi:

Tupigie kupitia **0800 11 00 19/20** bila malipo, au kupitia WhatsApp **0681 300 800**

LATRA

JINSI YA KUTUMIA MFUMO WA
LESENI ZA LATRA (RRIMS)

Maombi ya Cheti:

- Bofya ***Vyeti (maombi ya cheti)*** kisha ***Ongeza Maombi***, kisha jaza taarifa sehemu zilizo wazi (***Namba ya simu ianze na 255***),
- Hifadhi, na tuma maombi hayo, yakithibitishwa (Utaona neno ***CHETI HAI*** au ***ACTIVE***).

Maombi ya Leseni:

Baada ya kuthibitishwa, Bofya neno ***Leseni (Maombi ya Leseni)*** kisha ***Omba leseni (License Request)***, jaza taarifa za Chombo, aina ya leseni unayoomba, kisha thibitisha.

LATRA

JINSI YA KUTUMIA MFUMO WA
LESENI ZA LATRA (RRIMS)

- Fungua nukta tatu zilizopo kulia ya maombi yako na bofya neno ***Angalia Maombi*** ili uweke viambatisho

Viambatisho:

- ***Kadi ya chombo***
- ***Hati ya Bima***
- ***Hati ya Ukaguzi wa Polisi***

Wasilisha maombi kwa ajili ya hatua zingine, Maombi yako yatafanyiwa kazi na kutumiwa **Ankara ya malipo (Control number)** kwenye namba yako ya simu uliyotumia wakati wa kujisajili, pia unaweza kupata Ankarakwenye mfumo kwa kubofya neno ***Bili***

SSP KILEWA AWAONYA MADEREVA WANAOCHEZEA MFUMO WA VTS

SSP Nokter Kilewa, Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya (wa kwanza kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mha. Shaban Mdende, Afisa Mfawidhi Mkoa wa Mbeya (wa katikati) alipotembelea Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kilichopo Mikocheni, Dar es Salaam Agosti 6, 2025.

SSP Nokter Kilewa, Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya amewaonya madereva wanaochezea Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kuacha tabia hiyo mara moja kwani wanaweza kuchukuliwa hatua kali ikiwemo kufutiwa leseni zao.

SSP Kilewa amesema hayo kwenye mafunzo ya Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) yaliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Agosti 06 na 07, 2025, Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kilichopo Mikocheni, Dar es Salaam na Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli.

"Naishukuru sana LATRA kwa kutupatia mafunzo haya ambayo yanaenda kubadilisha utendaji kazi wetu kwa kuongeza ufanisi ukizingatia baada ya mafunzo haya tumeongeza wigo wa uelewa kuhusu mfumo huu unavyofanya kazi na hivyo tunafahamu namna bora ya kuutumia kwa kufuatilia magari yakiwa barabarani ili kupunguza ajali nchini," amesema SSP Kilewa.

Naye Bw. Geoffrey Silanda, Meneja Uratibu Usalama na Mazingira LATRA ameeleza namna mfumo wa VTS unavyofanya kazi ikiwa ni pamoja na kufuatilia na kutoa taarifa za magari kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa safari, na amebainisha faida za mfumo huo kuwa, tangu kuanzishwa kwake umesaidia kupunguza ajali zinazogharimu maisha ya watu na mali zao.

"Mafunzo haya ni sehemu ya mpango wa kitaifa wa kuwajengea uwezo Wakuu na Warakibu wa Jeshi la Polisi Kikosi

Inaendelea >>> Uk 14

SSP KILEWA AWAONYA MADEREVA WANAOCHEZEA MFUMO WA VTS

<<< Inatoka Uk 13

cha Usalama Barabarani mikoa yote nchini ambapo hadi sasa, tumetoa mafunzo mkoa wa Dar es Salaam, Pwani na Mbeya," amesema Bw. Silanda.

Kwa upande wake, Bw. Mbwana Ndaro, Afisa Mfawidhi LATRA Kituo cha VTS amewaeleza maafisa hao namna wanavyoweza kutumia mfumo huo kupata taarifa zote za magari na kumtambua dereva anayekiuka Sheria na Taratibu za usafiri ardhini ikiwa ni pamoja na kuendesha gari kwa mwendo hatarishi, dereva kuendesha gari zaidi ya saa nane, kuchezewa kwa mfumo na kupata taarifa iwapo gari imepata ajali kwa kutumia mfumo huo.

Vilevile Bw. Ndaro ameelezea kuhusu matumizi ya Kitufe cha Utambuzi wa Dereva (i-Button) kuwa, dereva anapaswa kukitumia anapowasha gari na wakati wote akiwa safarini na endapo gari litapata changamoto yoyote , ni rahisi kupata taarifa za dereva aliyekuwa anaendesha.

Mafunzo hayo ya siku mbili yametolewa na Bw. Geoffrey Silanda, Meneja Uratibu Usalama na Mazingira LATRA, Bw. Mbwana Ndano, Afisa Mfawidhi LATRA Kituo cha VTS na kuhudhuriwa na Mha. Shabani Mdende, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Mbeya, SSP Nokter Kilewa, Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya aliyeambatana na maafisa wengine watatu wa Jeshi Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Kitengo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari wa Mkoa huo.

tiketi.latra.go.tz/ Appstore/ Playstore

- **Ni lango la tiketi za Mabasi yote na Treni**
- **Abiria fanya wekesho (booking) na kulipia Tiketi**
- **Inapatikana kwa Simujanja, Wakala wa Benki**
- **Kumbuka:**
  Abiria hakikisha Tiketi yako ina taarifa zako muhimu kama vile jina kamili, namba ya simu, unapotoka, Kituo unachokwenda na namba ya kiti utakachokaa (nafasi katika basi au treni)

Pamoja kwa Usafiri Bora

PROF. KAHYARARA: KAMPUNI ZA TIKETI MTANDAO ZINAUNGANISHA MIFUMO YAO NA YA SERIKALI

Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi ameitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuhakikisha wamiliki wa mifumo ya Tiketi Mtandao nchini wanaunganisha mifumo yao na Mfumo Jumuishi wa Mauzo ya Tiketi unaofahamika kwa jina la Safari Tiketi kwa kuwa ni jambo la kisheria na Kikanuni.

Prof. Kahayarara amesema hayo alipotebelea jengo la LATRA katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) Dar es Salaam, Julai 05, 2025. Amesema kuwa, uunganishaji wa mifumo ya tiketi mtandao na Mfumo Jumuishi wa Serikali ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Nakumbuka Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akizindua treni ya kisasa pale Dodoma, alitoa maelekezo nane na mojawapo ni hili la kuwa na Mfumo Jumuishi wa Tiketi Mtandao. Tunafurahi kwamba LATRA wameliwezesha hili na mfumo huu unamwezesha abiria kukata tiketi za mabasi pamoja na treni za kisasa (SGR) na za reli ya kati (MGR) kwa urahisi kwa njia ya mtandao,"amesem Prof. Kahyarara.

Prof. Kahyarara ameongeza kuwa, Mfumo wa Safari Tiketi unasaidia wamiliki wa mabasi kupata mapato yao papo hapo na pia unarahisisha ufuatiliaji wa mabasi

Inaendelea >>> Uk 16

Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi (kushoto) akiwa na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA (kulia) alipotembelea Jengo la Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) lililopo viwanja vya Mwalim Julius Nyerere kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (Sabasaba) Julai 8, 2025.

PROF. KAHYARARA: KAMPUNI ZA TIKETI MTANDAO ZIUNGANISHE...

<<< Inatoka Uk 15

yanayotoa huduma pamoja na kufahamu idadi ya abiria wanaosafiri.

Kwa upande wake, CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema ni kosa kisheria kuwa na mfumo wa kutoa tiketi mtandao bila kuthibitishwa na LATRA, pia, ametoa tahadhari kwa wamiliki wa mabasi kutotumia kampuni za tiketi mtandao zisizoidhinishwa na LATRA baada ya tarehe 14 Julai, 2025.

"Wamiliki nawatahadharisha msije mkaingia kwenye matatizo ya kuzuiliwa kutoa huduma kwa kuwa usipotoa tiketi mtandao, huruhusiwi kufanya kazi ya usafirishaji na pia haturuhusiwi kukupa leseni. Tumewapa taarifa za awali kuhusu kampuni ambazo hazijakamilisha utaratibu kwahiyo muwafuatilie na muhakikishe mnatumia kampuni zilizokidhi vigezo mara baada ya muda waliopewa kuisha," amesisitiza CPA Suluo.

Tarehe 02 Julai, 2025 Mamlaka ilitangaza kampuni tatu za Tiketi Mtandao ambazo mifumo yao imekidhi vigezo ambazo ni Otapp Agency Company Limited, Hashtech Tanzania Limited na Iyishe Company Limited na kampuni nyingine sita (06) ambazo ni AB Courier Express Limited, Busbora Company Limited, Logix Company Limited, Mkombozi Infotech Company, Sepatech Company Limited na Web Corporation Limited. zilizopatiwa siku 14 kushughulikia changamoto za mifumo yao ili kuidhinishwa.

Aidha Kampuni mbili Duarani Innovative Company na Itule Company zimebainika kuwa na changamoto na kukosa sifa za kutoa huduma ya Tiketi Mtandao na hivyo wamepewa siku (07) za matazamio na wakishindwa hawataruhusiwa kutoa huduma na wateja wao watashauriwa kuhamia kwa watoa huduma waliokamilisha utaratibu.

Kanuni ya 5 ya Kanuni za Tiketi Mtandao za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024 zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 20 la Januari 12, 2024 zimeweka vigezo vya kupata kibali ambavyo ni pamoja na mfumo husika kuwa na ulinzi dhidi ya uvamizi wa kimtandao na kuwa na uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya Serikali.

"Tunafurahi kwamba LATRA wameliwezesha hili na mfumo huu unamwezesha abiria kukata tiketi za mabasi pamoja na treni za kisasa (SGR) na za reli ya kati (MGR) kwa urahisi kwa njia ya mtandao."

Prof. Godius Kahyarara

LATRA, DCEA KUSHIRIKIANA KUDHIBITI USAFIRISHAJI WA DAWA ZA KULEVYA

Bw. Aretas Lyimo, Kamishna Jenerali Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya (wa katikati) akikabidhiwa zawadi na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA (kushoto) alipotembelea Jengo la Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) lililopo viwanja vya Mwalim Julius Nyerere kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaaam (Sabasaba) Julai 11, 2025, (wa kwanza Kulia) Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) zimepanga kushirikiana kutoa elimu ya namna bora ya kudhibiti vitendo vya usafirishaji wa dawa za kulevya kwa wamiliki wa mabasi ya masafa marefu, madereva na wahudumu (makondakta) ambao wamekuwa wakishiriki kwa kujua ama kutokujua kusafirisha dawa hizo kwenye mabasi.

Akizungumza alipotembelea jengo la LATRA kwenye maonesho ya 49 ya biashara ya kimataifa (Sabasaba) Bw. Aretas James Lyimo, Kamishna Jenerali DCEA amesema elimu hiyo inahusu Sheria ya kudhibiti dawa za kulevya na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini ili kuwaeleza kuhusu athari za kujihusisha na vitendo vya usafirishaji wa dawa za kulevya kwenye vyombo vya moto kibiashara.

"Tunatoa elimu kwa madereva, makondakta na wamiliki wa magari ili waelewe kwamba wanapokamatwa na dawa za kulevya kupitia basi au chombo cha moto anachoendesha, dereva na kondakta wanahusika moja kwa moja kwa kuwa wao wamepakia mzigo na ndio wenye dhamana na basi likiwa safarini hivyo wanapaswa kuelewa aina ya mzigo waliopakia kwenye basi lao,"

Inaendelea >>> Uk 18

LATRA, DCEA KUSHIRIKIANA KUDHIBITI USAFIRISHAJI WA DAWA ZA KULEVYA

<<< Inatoka Uk 17

ameeleza Bw. Lyimo.

Bw. Lyimo ameongeza kuwa, wamiliki wa mabasi wamekuwa wakilalamika pindi magari yao yanapokamatwa na dawa za kulevya hivyo kupitia elimu wataelewa kuwa basi nalo linahusika kwa kuwa ndio limebeba dawa hizo na ni kielelezo namba moja mahakamani

"Nawasihi wamiliki wa vyombo vinavyodhibitiwa na LATRA kuajiri madereva na wahudumu wenye uadilifu na wahakikishe wanaingia nao mkataba wa kukataza kubeba dawa za kulevya kwenye chombo kwa kuwa itakapobainika, wote watakuwa na hatia ya kusafirisha dawa hizo ambapo msafirishaji atapata kifungo cha maisha kutokana na kile alichokibeba au kifungo cha miaka 30 jela na chombo kilichobeba nacho kitataifishwa," amesema Bw. Lyimo.

Naye CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amewataka madereva na wahudumu wa vyombo vinavyodhibitiwa na LATRA kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria za nchi kwakuwa zimewekwa kwa ajili ya kulinda jamii.

Vilevile amesema LATRA inatoa leseni za usafirishaji zenye masharti yanayopaswa kuzingatiwa na msafirishaji ikiwemo vitu vinavyopaswa kusafirishwa, pia Sheria na Kanuni za Mamlaka zinaelekeza mhudumu kukagua mzigo kabla hajaweka alama

CPA Suluo vilevile amewasihi wasafirishaji kuajiri madereva waliothibitishwa na wahudumu waliosjiliwa na LATRA lakini pia wahakikishe wanakuwa na utamaduni wa kufanya kazi kwa maadili ikiwemo kukataza kubeba dawa za kulevya.

"Dereva na kondakta wanahusika moja kwa moja kwa kuwa wao wamepakia mzigo na ndio wenye dhamana na basi likiwa safarini hivyo wanapaswa kuelewa aina ya mzigo waliopakia kwenye basi lao,"

Bw. Aretas Lyimo

PROF. AME AWASIHI WASAFIRISHAJI KUAJIRI MADEREVA WENYE SIFA NA TABIA NJEMA

Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewasihi wasafirishaji nchini kuajiri madereva wenye sifa na tabia njema ili kusaidia kupunguza ajali barabarani.

Prof. Ame amesema hayo kwenye ziara ya Bodi ya Wakurugenzi LATRA kwa Kampuni ya Superdoll, Dar es Salaam Agosti 01, 2025,

Prof. Ame ameeleza kuwa, ni muhimu wasafirishaji wengine kujifunza kutoka kampuni ya Superdoll kuhusu namna wanavyowapata madereva wao kwa kuzingatia tabia (character), uwezo (competency) na namna dereva anaweza kufanya kazi na wengine (chemistry) ili kupata matokeo wanayotaka.

"Watoa huduma wengine nao kuna haja ya kujifunza kutoka Superdoll kwa kuwa wanafanya mambo makubwa ya usalama barabarani na wakiweza kutekeleza hata asilimia 20 tu ya wanayotekeleza kampuni hii itasaidia sana kupunguza ajali barabarani," amsema Prof. Ame.

Vilevile amesema, Superdoll ni kampuni iliyoweka kipaumbele na kuwekeza sana kwenye suala la usalama barabarani, hivyo wamejifunza mbinu mbalimbali ambazo watazitumia katika kuboresha na kujenga mifumo ya kiudhibiti.

"Tukitazama mfumo wao wa kufuatilia magari jinsi unavyoenda na muda, unamuona dereva

Inaendelea >>> Uk 20

Prof. Ahmed Mohamed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akizungumza kwenye kikao cha ziara ya Bodi ya Wakurugenzi LATRA kwa Kampuni ya Superdoll, Dar es Salaam Agosti 01, 2025.

PROF. AME AWASIHI WASAFIRISHAJI KUAJIRI MADEREVA WENYE SIFA NA TABIA NJEMA

<<< Inatoka Uk 19

na vitendo vyake akiwa safarini ambapo si tu mfumo unapeleka taarifa kwa wataalam wao lakini pia unamuarifu dereva kuhusu vitendo hivyo vinavyohatarisha usalama anavyofanya akiwa barabarani. Hii inasaidia sana kiusalama kwa kuwa dereva anajirekebisha papo hapo baada ya kukumbushwa na mfumo unaomuongelesha kwa sauti," amesema Prof. Ame.

Akizungumzia suala la kudhibiti uchovu wa madereva wawapo safarini, Prof. Ame amesema Superdoll wanatumia mfumo kusimamia uchovu wa dereva na kwa upande wa LATRA kwa sasa wanaandaa Kanuni na kupitia ushirikiano uliopo, Kampuni hiyo nayo itatakiwa kutoa maoni yao ili kupata Kanuni zitakazotatua changamoto hiyo.

Katika hatua nyingine, Prof. Ame amefafanua sababu ya Bodi ya LATRA kufanya ziara kwenye Kampuni hiyo, "Taarifa zetu zinaonesha kwamba Superdoll ni miongoni mwa wadau wetu wanaofanya vizuri sana kwa hiyo tukawa na ari kubwa ya kuja kumtembelea kwa lengo la kujifunza. Dira yao inaonesha wanataka kuwa wasafirishaji bora Afrika Mashariki na Kati lakini ukweli ni kwamba ni watoa huduma za usafirishaji wakubwa Afrika, hakuna wa kupinga, kampuni hii imetoa huduma kilomita milioni 45 bila kupata ajali".

"Watoa huduma wengine nao kuna haja ya kujifunza kutoka Superdoll kwa kuwa wanafanya mambo makubwa ya usalama barabarani

Prof. Ahmed Ame

Naye Bw. Ibrahim Juma, Meneja Mkuu Kampuni ya Superdoll amewasihi wasafirishaji kuwajengea uwezo madereva wao kwa kuwaongezea ujuzi kupitia mafunzo ili kuongeza tija na thamani yao katika kazi wanayoifanya na hatimaye kuwa na sekta ya usafirishaji yenye usalama.

Pia, ameishukuru Bodi ya LATRA na ameiomba kuendeleza ushirikiano uliopo ili kwa pamoja wafikie lengo la kuwa na sekta ya usafirishaji yenye tija na manufaa kwa Serikali, Wasafirishaji na Wananchi kwa jumla.

LATRA inautaratibu wa kuwatembelea wadau wake ili kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna bora ya kudhibiti sekta ya usafiri ardhini nchini kwa kuwa maendeleo ya sekta hii yanahitaji mchango wa kila mdau.

LATRA
IMETHIBITISHWA ISO 9001

LATRA YAASWA KUWAFIKIA WADAU VIJIJINI

Bw. Ezekiel Emmanuely, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Dodoma akitoa maelezo kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na LATRA kwa Bi. Happiness Sulle, Katibu Tawala Wilaya ya Mkalama - Singida alipo tembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nanenane Agosti 8, 2025 Dodoma.

Bi. Happiness Sulle, Katibu Tawala Wilaya ya Mkalama - Singida ameiasa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuendelea kutoa elimu kwa wananchi hasa waliopo vijijini ili kuwaongezea uelewa wa majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na LATRA.

Bi. Sulle amebainisha hayo alipotembelea banda la LATRA lililopo Viwanja vya Nzuguni, Dodoma kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nanenane yanayofanyika kuanzia Agosti 1 hadi 10, 2025 ambapo alielezwa majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na LATRA katika sekta ya usafiri ardhini nchini.

"Nawasihi kuendelea kutoa elimu hadi ngazi za vijijini ili kuwafikia wananchi wengi zaidi, ili wafahamu kazi, majukumu yenu na hatimaye waweze kutumia vizuri huduma za usafiri ardhini. Pia mnapaswa kuongeza ubunifu ili kuendana na teknolojia ya sasa katika utekelezaji wa majukumu yetu," amesema Bi. Sulle.

Vilevile ameipongeza LATRA kwa jitihada za kuboresha sekta ya usafiri ardhini zinazochagiza mapinduzi katika usimamizi wa huduma za usafiri nchini hasa kupitia mifumo ya kidigitali.

Kwa upande wake Bw. Ezekiel Emmanuely, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Dodoma amesema, "LATRA inatambua umuhimu wa kuwafikia wananchi kwa kutoa elimu ya moja kwa moja, maonesho haya ya Nanenane ni jukwaa muhimu la kufikia wananchi kwa kuwaelimisha kuhusu haki, wajibu na huduma bora za usafiri ardhini."

Naye Mha. Dkt. Prosper Mgaya,

Inaendelea >>> Uk 22

LATRA YAASWA KUWAFIKIA WADAU VIJIJINI

<<< Inatoka Uk 21

Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), ametembelea banda la LATRA na amejifunza kuhusu Mifumo inayotumiwa na LATRA katika shughuli za udhibiti na ameeleza namna NIT inavyoshirikiana na LATRA katika kuboresha sekta ya usafiri nchini.

"Ushirikiano kati ya NIT na LATRA unaendelea kuleta manufaa makubwa katika sekta ya usafiri hasa kwa kutoa wataalamu waliobobea katika usimamizi na udhibiti wa usafiri ardhini na leo nimejifunza Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) ambao unamrahisishia abiria kupata taarifa mbalimbali za mabasi yanayowasili katika vituo vya mabasi pamoja na kutambua mwenendo wa basi linapokuwa safarini, hii inadhihirisha ubunifu wenu mkubwa kupitia mifumo ya kidijiti," amesema Mha. Dkt. Mgaya.

LATRA inashiriki katika maonesho haya kwa kuonesha mchango wa sekta ya usafirishaji katika kufanikisha maendeleo ya kilimo na biashara nchini, kupitia udhibiti bora wa usafiri wa mazao, pembejeo na watu vijijini na mijini.

Bi Nancy Amani, Afisa Uhusiano na Mawasiliano - LATRA akielezea kazi na majukumu ya LATRA kwa wanafunzi waliotembelea banda la LATRA kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nanenane Agosti 8, 2025 Dodoma.

LATRA
IMETHIBITISHWA ISO 9001

Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) (kulia) akisikiliza maelezo kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na LATRA wakati alipotembelea banda la LATRA kwenye Kongamano la Tatu la Kimataifa la Uchukuzi na Lojistiki lililoandaliwa NIT Ukumbi wa Mlimani City Dar es Salaam Agosti 21, 2025.

Maafisa usafirishaji wa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Maafisa Usafirishaji wa Pikipiki Dar es Salaam (MAUPIDA SACCOS), wakiwa kwenye hafla ya kukabidhiwa Cheti cha Uwakala wa Kutoa Leseni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Agosti 13, 2025, ukumbi wa Golden Jubilee, Dar es Salaam.

Mdau wa usafirishaji akipatiwa elimu kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) alipotembelea Jengo la LATRA viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba)

LATRA

IMETHIBITISHWA ISO 9001

Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mwasiliano, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Likiongozwa na Bodi ya Wahariri.

Mwenyekiti: **CPA HABIBU SULUO** | Mhariri Mkuu: **SAMUEL KEENJA** | Wahariri Wasaidizi: **SALUM PAZZY**, **MAMBWANA JUMBE** | Waandishi: **MAMBWANA JUMBE**, **NANCY AMANI** na **MARYAM NINA** | Msanifu Jarida: **IBRAHIM SAID** na **DEUSDEDITY MASEMBA**